



Kumfuata Yesu huko UINGEREZA

KUTANA NA
LUCIA, VIVIE
NA ZAC!



Kuwahusu Wao

MAJINA: Lucia, umri miaka 7; Vivie, umri miaka 9; na Zac, umri miaka 9

KUTOKA: Herefordshire, Uingereza

LUGHA: Kiingereza

MALENGO NA NDOTO: Kuwa rafiki mwema (Lucia), kukariri Makala ya Imani (Vivie) na kuwasaidia watoto kucheza michezo (Zac)

FAMILIA: Lucia na Zac ni kaka na dada na Vivie ni binamu yao.



Je, Ni kwa Namna Gani Wao Wanamfuata Yesu

"Familia zetu zinaishi kwenye shamba moja na Bibi na Babu," Lucia anasema. "Kuna kazi nyingi za kufanya, lakini tunahisi vizuri wakati tunapotumikia. Tunajua kwamba Yesu Kristo anatutaka tutumikie."

"Tunamsaidia Bibi kuwatunza farasi wadogo," Vivie anasema. "Tunawaongoza kondeni kulisha. Tunasafisha zizi la farasi, kuchana manyoya yao, kuwalisha na kujaza ndoo zao za maji. Tunapenda kumsaidia Bibi."

Zac humfuata Yesu kwa kutumikia pia. "Babu mkuu wetu alifanyiwa upasuaji kwenye mkono wake. Hangeweza kutunza bustani lake. Familia yangu, binamu, akina babu na bibi walisaidia kufyeka nyasi na kuondoa magugu. Babu mkuu alikuwa na furaha sana!" ●

VIELEZO NA LUCY SEMPLE DEAKIN



Je, Ni kwa Namna Gani Unamfuata Yesu?

Kuna njia nyingi za kumfuata Yesu. Je, ni kwa namna gani wewe unamfuata Yeye? Andika na utuelezee!

Mapendeleo Yao

HADITHI YA MAANDIKO: Anachopenda Zac ni wakati Yesu alitembea juu ya maji



MAHALI: Lucia na Vivie wanapendelea kuwa na farasi



TUNDA AU MBOGA: Maembe (Lucia), viazi vitamu (Vivie), brokoli (Zac)



SOMO SHULENI: Sanaa (Lucia na Vivie) na historia (Zac)



RANGI: Zambarau (Lucia), feruzi (Vivie) na njano (Zac)